**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**CHUO CHA UFUNDI STADI CHA WILAYA YA KARATU (KARATU DVTC)**

**Ref. VETA/KRT/T.02/06**

**Ndugu:**.........................................................................................

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUND STADI CHUO CHA VETA KARATU**

Husika na mada tajwa hapo juu

2. Hongera kwa kuchaguliwa kwa kujiunga na Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Karatu (KARATU DVTC).

3. Umechaguliwa kujiunga na fani iliyowekwa vema hapo chini

   1. **Plumbing and Pipe Fittings (PPF)** ☐
   2. **Electrical Installation (EL)** ☐
   3. **Design, Sewing and Cloth Technology (DSCT)** ☐

4. Chuo kitafunguliwa rasmi mnamo tarehe 13/01/2025 na utapaswa kufika chuoni saa mbili kamili asubuhi (02:00) ukiwa na mahitaji muhimu kama yalivyoonyeshwa kwenye kiambatanisho 1 - 7.

5. **Tafadhali fuata maelekezo yote yaliyoelekezwa kwenye viambatanisho.**

6. Nakutakia maandalizi mema na karibu sana Chuo cha VETA cha Wilaya ya Karatu

Stanslaus Ntibara
**MKUU WA CHUO**

***Barua zote rasmi zipitie kwa Mkuu wa Chuo cha VETA Wilaya ya Karatu***

Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Karatu
40 Kitongoji cha Umbe
Kijiji cha Bashay
23609 Qurus
Karatu, Arusha

Karatu District Vocational Training Centre – KDVTC
S.L.P 352,KARATU-ARUSHA.TANZANIA Simu: +255 755 000 040
Barua pepe: karatudvtc@veta.go.tz, Tovuti: www.veta.go.tz

## 1.0 MAHALI KILIPO NA NAMNA YA KUFIKA CHUONI

1.1 Chuo cha Ufundi Stadi cha VETA Wilaya ya Karatu, (KARATU DVTC) ni taasisi inayomilikiwa na Mamlaka ya Elim una Mafunzo ya Ufundi Stadi(veta) katika Kijiji cha Bashay. Chuo kipo chini ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

1.2 Karatu DVTC, kipo Mkoa wa Arusha katika Wilaya ya Karatu. Chuo Kipo katika Kijiji cha Bashay takriban Kiomita sita (06) kutoka Karatu mjini uelekeo wa lilipo geti la Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro.

1.3 Kutoka Karatu mjini unaweza kufika Karatu DVTC KWA USAFIRI WA GARI BINAFSI, bajaji n ahata pikipiki (bodaboda)

1.4 Endapo utahitaji msaada au maelezo zaidi tafadhali wasiliana na **Mratibu wa Mafunzo** kwa namba **0673 466 030** au `**Matron'** kwa namba **0758 701 163**

***Karibu sana Chuo cha Ufundi Stadi Wilaya ya Karatu***

**Kiambatisho Na. 1**

## 2.0 MAHITAJI MUHIMU

- Cheti halisi cha kidato cha nne au Cheti cha Darasa la Saba kwa ambao hawakufanikiwa kufika kidato cha nne (Original academic certificate / Results slip) na nakala yake (photocopy). Baada ya cheti kuthibitishwa na Msajili/Dawati la kujiandikisha , utaruhusiwa kuondoka na cheti chako halisi na nakala kubaki chuoni kwa kumbukumbu . Kumbuka: **Living Certificate / copy havikubaliwi.**
- **Zingatia usalama** . Unatakiwa kujinunulia" safety Boots" yenye sifa zifuatazo - Slip toe cap: oil resistance sole. (Wanafunzi wa ushonaji nguo hawahusiki) Ikiwa huna uhakika na maelezo yoyote, fika chuoni Ofisi ya msajili kwa ufafanuzi.
- Mashati mawili meupe (Mikono mifupi) ya Tetroni
- Suruali mbili (02) rangi ya Dark Blue - zingatia vipimo ulivyopewa.
- Jozi moja (01) ya viatu vyeusi vya ngozi
- Vifaa vya hesabu (Mathematical set) Kalamu na panseli
- Daftari kumi (10 )aina ya 'counter book quire four '(4)
- Sweta moja (01) ya Dark Blue Mavazi ya heshima na vifaa vya usafi binafsi
- Ovaroli kwa fani ya electrical Installation, Plumbing and pipe fittings na ovakoti kwa fani ya ushonaji – Rangi ya Dark Blue
- Bima ya afya (NHIF) unapaswa kuja na kitambulisho chako cha bima ya afya kama una bima au kiasi cha shilingi 50,400 kwa wasio na bima.
- Godoro kwa wanafunzi wa Bweni (kipimo mita 2.5)
- Phocopy paper ream 1
- Fyekeo 1, Jembe1, Reki1
- Blanket, Mashuka mawili rangi ya Blue, Neti ya Mbu, Ndoo ya Kuogea/kufulia, kikombe na kijiko.

**Kiambatisho Na. 2**

## 3.0 MPANGILIO WA ADA NA MALIPO MENGINE – FEE STRUCTURE

## CHUO CHA UFUNDI STADI CHA WILAYA YA KARATU (KARATU DVTC)

## (FEE STRUCTURE)

### 3.1 UTANGULIZI

Ada kwa mwanachuo wa bweni ni shilingi laki moja na elfu ishirini tu (120,000/=) kwa mwaka na mwanachuo wa kutwa ni shilingi elfu sitini tu (60,000/=) kwa mwaka. Yapo mahitaji mengine ya muhimu ya kila mwanachuo ili kushiriki vyema katika mafunzo kwa kila mwanachuo anapowasili/kuripo chuoni. Tafadhali zingatia maelezo unayopewa katika ulipaji wa ada yako.:-

### 3.2 JEDWALI LA MALIPO

| NAMBA | MAHITAJI | KUTWA (MWAKA WA I) | | BWENI (MWAKA WA II) | | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Awamu ya kwanza** | **Awamu ya pili** | **Awamu ya kwanza** | **Awamu ya pili** | |
| 01 | ADA YA MAFUNZO | 30,000 | 30,000 | 60,000 | 60,000 | Malipo ya ada yafanywe kwa control namba utakayopewa na ofisi ya uhasibu |
| 02 | NEMBO YA VETA 1PC | 5,000 | - | 5,000 | - | Malipo haya yanatakiwa kulipwa kwa control namba. |
| 03 | TAHADHARI | 10,000 | - | 10,000 | - | |
| 04 | KITAMBULISHO | 5,000 | - | 5,000 | - | |
| 05 | MICHEZO | 10,000 | - | 10,000 | - | |
| 06 | TISHETI | 18,000 | - | 18,000 | - | |
| 07 | MAHAFALI | 25,000 | - | 25,000 | - | |
| 08 | SERIKALI YA WANAFUNZI | 5,000 | - | 5,000 | - | |
| 09 | FEDHA YA GODORO | | - | 25,000 | - | |
| | | **108,000** | **30,000** | **163,000** | **60,000** | |

**Kiambatisho Na. 3**

### 3.4 UTARATIBU WA MALIPO

Ada italipwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza itafanyika Januari, 2025. Nusu ya Ada unapoingia na nusu iliyobakia muhula wa pili Julai, 2024 kwa bweni au kutwa. Au ada yote unapoingia chuoni 2024. Gharama kwa mahitaji mengine zitalipwa

***NB: Mwanafunzi hatopokelewa kama hakutimiza kiasi hicho.***

### 3.5 NAMNA YA KULIPA ADA

Mwanachuo afike Chuoni VETA Karatu na atapewa namba ya Malipo ya serikali (control number) ya kulipia

### 3.6 BIMA YA AFYA.

Kila mwanachuo anatakiwa kuwa na bima ya afya ya NHIF. Endapo atakuwa ana Bima yake ya afya aje nayo, na kama hatakuwa hana Bima ya Afya aje na fedha Tshs 50,400/= kwa ajili ya kukatiwa Bima ya afya ya NHIF, na endapo hatotekeleza hayo, mwanafunzi hatopokelewa hapa Chuoni. **Zingatia** kwa wanafunzi wa bweni pekee.

### 3.7 KUPOKELEWA.

Waliolipa Ada kamili, bima ya afya na vifaa vilivyotajwa na kutimiza masharti yote yaliyoandikwa hapo juu, **NDIO WATAPOKELEWA CHUONI**. Utatakiwa kuonyesha vitu hivi kwa Walimu wa dawati la usajili wa wanachuo utakaporipoti na utapewa kibali cha usajili ili kupokelewa katika fani yako na Bwenini.

**Kiambatisho Na. 4**

### 4.0 SHERIA ZA CHUO

**4.1 KUFIKA CHUO KWA WAKATI**

Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1:00 asubuhi. Hii inamaana ifikapo saa 1:00 asubuhi wanafunzi wote wanatakiwa wawe wameshafika chuoni. Adhabu kali itatolewa kwa wachelewaji.

**4.2 RUHUSA YA KUWA NJE YA CHUO**

Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani, hospitali au sehemu nyingine yoyote ile bila ya kuruhusiwa na mwalimu wa zamu kupitia kwa mwalimu wa darasa.

Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima habari au taarifa zifike chuoni, bila ya kufanya hivyo ni kosa.

Mahudhurio chini ya 85% mwanafunzi atanyimwa cheti cha kuhitimu mafunzo.

Vyumba au Madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora/kuandika kuta, au kuweka miguu kwenye kuta za majengo ya chuo.

**4.3 MAVAZI**

Sare ya chuo ni suruali ya bluu na shati jeupe la mikono mifupi na T-shirt ya VETA. Sare hiyo ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo chuoni na wakati wa safari ya kuja chuoni nakurudi nyumbani. Wakati wote shati liwe limechomekewa.

Ovaroli livaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.

Viatu vyenye visigino virefu na kandambili au viatu vya wazi (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni.

**4.4 USAFI WA MWILI**

Hairuhusiwi kuvaa hereni, pete, bangili na mapambo ya aina yoyote ile kwa kipindi chote cha mafunzo. Pia hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kali.

**4.5 NYWELE KWA WAVULANA:**

Zikatwe ziwe fupi sana, **KIPARA** hakiruhusiwi kabisa. Ndevu haziruhusiwi. Ndevu za aina zote haziruhusiwi mustachi/sharubu.

**4.6 NYWELE KWA WASICHANA:**

Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma. Kucha zisifugwe kabisa wala kupakwa rangi.

**Kiambatisho Na. 5**

### 4.5 WIZI WA MALI ZA CHUO AU MALI YA MTU YEYOTE YULE

Vitendo vyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika kuwa mwanafunzi ameiba mali ya chuo au mwanafunzi mwenzake, basi atafukuzwa chuo mara moja.
Ukipoteza kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa na ukakinunue kifaa chenyewe au ulete mbadala ya ulichokipoteza.
Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo.
Mwanafunzi atapekuliwa wakati wakutoka karakana na getini.

### 4.6 UGOMVI

Ugomvi kupigana au kushambuliana ni makosa ya jinai. Atakayepatikana akijihusisha na matendo ya namna hiyo atafukuzwa chuoni nakukabidhiwa kwenye vyombo vya dola.

### 4.7 ULEVI

Iwapo itabainika mwanafunzi analewa au kuonekana katika sehemu ya vileo, anavuta bangi au madawa ya kulevya adhabu yake ni kufukuzwa chuo mara moja.

### 4.8 MAPENZI

Mahusiano ya kimapenzi chuoni kati ya mwanachuo na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi/mwalimu na mwanafunzi hairuhusiwi kabisa.
Mwanachuo wa kiume au wakike haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi watumishi bila ya kibali au ruhusa.

### 4.9 MIGOMO

Migomo ni marufuku, na kuchochea migomo ni kosa lisilo stahimilika. Atakayeshawishi au kusababisha migomo atafukuzwa chuoni mara moja.

### 4.10 LUGHA

Lugha inayotumika kuendesha masomo ni kiingereza hivyo ni wajibu wa kila mwanachuo kujifunza kiingereza. Jina libadilishwe mpaka ziwepo sababu na hati maalum kwa uthibitisho na ajulishwe mkuu wa chuo mara moja. Ni marufuku kuwasha simu za mkononi wakati wote wa vipindi.

### 4.11 ONGEZEKO LA SHERIA KWA WANACHUO WA BWENI

Mwanachuo ataruhusiwa kutok anje ya chuo siku zifuatazo tu:-
Jumapili kuanzia saa 12:00 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni. Jumamosi kuanzia saa 7:30 mchana mpaka 12:00 jioni. Hairuhusiwi kutoka nje ya chuo wakati wowote bila kibali maalum. Mwanachuo yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya eneo la chuo anapaswa kuwa na kitambulisho cha chuo na atajiandikisha lango kuu akiwaamevaa sare ya chuo. Mwanachuo atakayeonekana maeneo ya nje ya chuo bila kitambulisho atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa nafasi ya kulala bwenini au kufukuzwa chuoni.
Mwanachuo atakayepatikana na kosa la kulala au kuwa nje ya chuo bila kibali atasimamishwa masomo.

### 4.12 KUPIKA CHAKULA BWENINI

Hairuhusiwi kupika chakula bwenini, na atakayekiuka hatua kali za sheria zitachukuliwa.

### 4.13 KUTEMBELEANA BWENINI NA NYUMBA ZA WAFANYAKAZI

Ni marufuku wanachuo wa kiume na wa kike kutembeleana mabwenini. Hairuhusiwi **KABISA** kwa mwanachuo kuingia katika eneo wanamoishi wafanyakazi wachuo bila ruhusa au kibali.

### 4.14 CHAKULA BWENINI

Hairuhusiwi kupeleka chakula bwenini. Endapo kuna mgonjwa, ruhusa maalumu kutoka kwa mwalimu wa zamu itatolewa.

### 4.15 TAA ZA DARASANI NA BWENINI

Taa za madarasani na mabwenini zizimwesaa 4:00 za usiku.

### 4.16 MGENI BWENINI

Hakuna ruhusa kumkaribisha au kumlaza mgeni, ikiwa mwanachuo atatembelewa na mgeni au Ndugu siku ya masomo ni lazima kumjulisha mwalimu wa zamu kabla ya kumkaribisha katika sehemu ya mazungumzo.

Wageni wanaruhusiwa kuwatembelea ndugu zao kila Jumamosi kuanzia saa 7:00 mchana hadi 12:00 jioni.
Kila Jumapili na siku za sikukuu kuanzia saa 12:00 asubuhi mpaka saa 12:00 za jioni.
Ruhusa ya kulala nje ya mipaka ya chuo itatolewa na ofisi ya mkuu wa chuo.

## 4.17 RUHUSA YA KULALA NJE YA CHUO

Ruhusa ya kutoka chuoni Jumamosi ni kuanzia saa 7:30 mchana hadi 12:00 jioni.
Jumapili na siku za sikukuu saa12:00 asubuhi hadi 12:00 jioni.
Majina yaandikwe kwenye kitabu cha kutoka na kuingia. Mhusika aweke muda wa kutoka na muda wa kurudi ,na ahakikishe amesainiwa mara tu anaporudi.

**CHUO CHA UFUNDI STADI CHA WILAYA YA KARATU (KARATU DVTC)**

---

## MEDICAL EXAMINATION FORM

**DATE …………………………………**

**THE MEDICAL OFFICER**

…………………………………………………

…………………………………………………

…………………………………………………

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Name of trainee ………………………………………………………………………………………………..

Please examine the above named trainee to his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/an …………………………………………………………………………………………

Eye sight …………………………………………………………………..

Hearing …………………………………………………………………..

Asthma …………………………………………………………………..

Other serious diseases …………………………………………………………………..

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for training as above

Date ………………………………………… Designation …………………………………………………Signature and official stamp ……………………….

**Kiambatisho Na. 6**

## 5.0 KUKUBALI KUJIUNGA NA CHUO

Tafadhali jaza fomu ya kuridhia kujiunga na mafunzo hapo chini kisha ikabidhi kwa Msimamizi wa Mafunzo wakati wa usajili

Mimi …………………………………………………………… Fani ya ………………………………………………………..
Ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa pamoja na kuzingatia sharia na kanuni za chuo ambazo nimezisoma na kuzielewa vizuri.
Sahihi …………………………….. Tarehe ……………………………….
MDHAMINI
Mimi ………………………………………………………………… ambaye ni (Mzazi/Mlezi/Kaka/Dada n.k) ………………………………………………………………… Wa mtajwa hapo juu nathibitisha kuwa ninamdhamini nanitalipia gharama zote za mafunzo ikiwa ada pamoja na michango mingine kama ilivyoelezwa katika maelezo ya kujiunga na chuo wakati wote wa mafunzo.
Simu namba ……………………………………….
Sahihi …………………………….. Tarehe ……………………………….